

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA

Barua zote zitumwe kwa:

Simu: +255 27 2508073/2503494 (Director)

+255 27 2544330 (General)

Nukushi: +255 27 2545768

Unapojobu tafadhali taja:



Mkurugenzi wa Jiji

S. L. P. 3013,

20 Barabara ya Boma,
23101 ARUSHA,

Barua Pepe: cd@arushacc.go.tz

Tovuti: www.arushacc.go.tz

**MKURUGENZI WA JIJI LA ARUSHA ATOA UFAFANUZI KUKANUSHYA
TUHUMA ZA UWEPO WA AKAUNTI FEKI ILIYOTUMIWA NA CCM
KUIBA MILIONI 40**

Mnamo tarehe 19/8/2016 ilisambazwa taarifa ya uongo kwenye mitando ya kijamii ambayo kwa kiasi kikubwa ilipotosha Umma wa Watanzania kwamba Halmashauri ya Jiji la Arusha imegundua Akaunti feki iliyotumiwa na CCM kuiba milioni 40. Tungependa wananchi waelewe kwamba taarifa hiyo si sahihi na inapotosha Umma.

Halmashauri ya Jiji la Arusha ilipandishwa hadhi ya kuwa Jiji mwaka 2012 ambapo iliongezewa maeneo ili kukidhi vigezo vya hadhi hiyo. Kijiji cha Terrat ni mionganini mwa maeneo yaliyohamishiwa katika Jiji kutoka Halmashauri ya Arusha DC

Kwa mujibu wa taratibu za Serikali za Mitaa, Kijiji kina Mamlaka kama Serikali kamili na kina uwezo wa kufungua akaunti na kusimamia matumizi ya fedha zake.

Halikadhalika hakuna kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilichoketi na kujadili suala la kuihusisha CCM na wizi wa fedha za mnara wa Vodacom katika Kijiji cha Terrat kama ilivyoripotiwa na mtandao mmojawapo wa kijamii hapa nchini.

Napenda kuwaarifu watanzania wote kuipuuzia habari hiyo kwani haina ukweli wowote na nachukua nafasi hii kukanusha kwamba hakuna fedha zozote iliyochukuliwa na CCM katika Jiji la Arusha.

Imetolewa na:

Athuman J. Kihamia
**MKURUGENZI WA JIJI
ARUSHA
22.08.2016**